

# Ukatili wa kijinsia ni nini?

Kulingana na tafsiri iliyotolewa na Umoja wa Mataifa; "ukatili wa kijinsia" ni kitendo chochote anachofanyiwa mtu yeyote awe mwanamke, mwanaume au mtoto, kinacholenga kumuumiza kimwili au kiutu. Ingawa ukatili wa kijinsia anaweza kufanyiwa mtu yeyote, kundi la wanawake na watoto ndio wahanga wakubwa wa ukatili huu. Ukatili huu haukubaliki na ni kosa kisheria

## Mifano ya ukatili wa Kijinsi ni kama:



Kupigwa




Kubakwa



Ndoa za utotoni



Kutukanwa



Kudhalilishwa kingono



Kudhalilishwa kihisia

## Tunafanya nini kama jamii?

- Kuwalinda wasichana na wavulana dhidi ya unyanyasaji na ukatili kwa kuwaelimisha kuhusu ni wapi wanaweza kutoa taarifa na kupata msada wa haraka ikiwemo kutoa taarifa katika madawati ya jinsia katika vituo vya polisi, vituo vya afya, kwa mjumbe wa nyumba kumi au serikali za mitaa.au hata kwa jirani mwema.
- Kusema ukweli kwa walimu au wazazi tukiona mtoto au kijana anafanyiwa ukatili au unyanyasaji.
- Kusaidiana wakati wa ukame au mvua nyingi na mafuriko tukizingatia athari zinazoweza kuwapata wasichana na wanawake, watoto, vijana na hata watu wenye ulemavu.
- Kutunza mazingira yetu ya shule hata nyumbani kwa kupanda miti, na kutumia maji kwa uangalifu.

Mradi wa **Kesho Njema** umefadhiliwa na **Ubalozi wa Ireland Tanzania** na kutekelezwa na **MyLEGACY**

MyLEGACY Urithi Wangu

Government of Ireland International Development Programme

MyLEGACY (Urithi Wangu) +255 764 574 099 info@mylegacy.or.tz www.mylegacy.or.tz
Target Complex House (No: 15), Mbezi Beach (Mskiti Street) Dar es Salaam, Tanzania

MyLEGACY Urithi Wangu

Government of Ireland International Development Programme

# "Tuishi Salama na Mabadiliko ya Tabianchi"



@mylegay.or.tz



# Mabadiliko ya Tabianchi ni nini?

Ni hali ya hewa kubadilika. Mvua kunyesha bila  mpangilio, joto kali sana, au ukame wa muda mrefu.




## Nini kinatokea tukikumbwa na mabadiliko ya tabianchi?

- Mvua nyingi yenye kupelekea mafuriko
- Ukame  wenye kusababisha njaa baada ya mashamba  kukauka
- Kukosekana maji safi na salama kwa binadanu na mifugo



## Wasichana na wavulana huathirika vipi?

- Wasichana wanatembea umbali mrefu kutafuta maji
- Wasichana wengine wanaolewa mapema
- Wavulana hufanya kazi ngumu mashambani, kwenye migodi, kupasua mawe na kubeba mizigo
- Baadhi ya wasichana na hata wavulana hulazimika kuacha shule kusaidia familia



# Afya ya uzazi ni nini?

Ni hali ya kuwa salama, kimwili, kiakili na kijamii na sio tu hali ya kutokuwa na ugonjwa au ulemavu katika masuala yote yanayohusiana na afya na mfumo wa uzazi.




## Nini maana ya Kubalehe?

Balehe ni kipindi cha mpito kutoka utoto kwenda utu uzima, ambacho mtoto hupitia mabadiliko ya kimwili, kihisia na kihomoni — na huashiria mwanzo wa uwezo wa kijinsia na uzazi. Kipindi hiki vijana huhitaji msaada wa wazazi na walimu kuelewa mabadiliko ya miili yao. Wasichana wanahitaji msaada wakati wa hedhi na pia kujiweka. safi na kupata huduma za afya.

## Hedhi ni nini?

Hedhi ni kipindi ambacho wanawake au watoto wa kike waliokwisha kubalehe hutokwa na damu ukeni. Hedhi ni sehemu ya asili katika mwili wa mwanamke au msichana na huashiria mabadiliko katika mwili wa wanawake au wasichana ambayo hutayarisha viungo vya uzazi vya mwanamke au msichana kuwa tayari kubeba ujauzito/ mimba.

